**MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAM YA (CMT) HALMASHAURI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU KUANZIA MWEZI JANUARI-MACHI, 2021 KILICHOFANYIKA TAREHE 08.04.2022.**

MAHUDHURIO YA WAJUMBE

| NA. | JINA | CHEO/WADHIFA | NAFASI |
|---|---|---|---|
| 1. | JOHN B. CHAO | KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W) | MWENYEKITI |
| 2. | JOYCE J. MASOGA | KAIMU AFISA UTUMISHI (W) | KATIBU |
| 3. | MWAHIJA CHINGOLOMBWE | KAIMU AFISA ELIMU SEKONDARI (W) | MJUMBE |
| 4. | REGAN D. MPUMBA | KAIMU AFISA MIPANGO (W) | MJUMBE |
| 5. | PAUL G. MKOMA | KAIMU AFISA ELIMU MSINGI (W) | MJUMBE |
| 6. | IRENE ASSEY | KAIMU MGANGA MKUU (W) | MJUMBE |
| 7. | NOHNY J. KIGODA | KAIMU AFISA USAFI NA MAZINGIRA (W) | MJUMBE |
| 8. | GEOFREY KIBESA | KAIMU MWEKA HAZINA (W) | MJUMBE |
| 9. | FRED Y. LOTTI | KAIMU AFISA MAENDELEO YA JAMII (W) | MJUMBE |
| 10. | GEOFREY NGULI | KAIMU AFISA MANUNUZI NA UGAVI (W) | MJUMBE |
| 11. | GILBERT M. KALANDA | KAIMU AFISA SHERIA (W) | MJUMBE |
| 12. | SHAIB B. PONERA | KAIMU AFISA ARDHI NA MALIASILI (W) | MJUMBE |
| 13. | CHRISTOPHER W. GHUMPI | KAIMU AFISA KILIMO NA USHIRIKA (W) | MJUMBE |
| 14. | SEVERINE M. MZELOO | KAIMU AFISA UCHAGUZI (W) | MJUMBE |
| 15. | VALENCE KILASARA | KAIMU MRATIBU TASAF (W) | MJUMBE |
| 16. | OMARI S. LIBUI | MTHIBITI UBORA SHULE (W) | MJUMBE |
| 17. | ELIUTHA A. KIDENYA | AFISA TARAFA-ITIGI | MJUMBE |

SEKRETARIETI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | CONSTANTINE MIHAMBO | MWANDISHI WA KIKAO |
| 2. | ADRIANA S. SIPPI | MWANDISHI WA KIKAO |

AGENDA ZA KIKAO

1. KUFUNGUA KIKAO.
2. KURIDHIA AGENDA.
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAM (CMT) CHA TAREHE 09.03.2022.
4. YATOKANAYO NA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAM (CMT) CHA TAREHE 09.03.2022.
5. KUSOMA NA KUREKEBISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA KAMATI MBALIMBALI.
6. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI MACHI, 2021.
7. TAARIFA ZA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI-MACHI, 2021).
8. OMBI LA KIBALI CHA AJIRA YA KUJITOLEA.
9. MAPENDEKEZO YA UTEUZI WA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.
10. MAPENDEKEZO YA KUBADILISHA JINA LA JIMBO LA UCHAGUZI.
11. TAARIFA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MFUKO WA AFYA WA PAMOJA (HSBF) NA UNICEF KWA AJILI YA VYETI VYA WATOTO.
12. KUFANYA MABADILIKO YA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI ILI KUJENGA NYUMBA YA MKURUGENZI YENYE GOROFA MOJA.
13. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI NYUMBA ZA WATUMISHI.
14. OMBI LA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA TSHS 13,661,988.00.
15. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU 2021/2022.
16. TAARIFA YA HALI YA USALAMA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI-MACHI, 2022.
17. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.
18. KUFUNGA KIKAO.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOL II/NA.115/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao, Mwenyekiti aliwasalimu Wajumbe na kuwakaribisha katika kikao ambapo aliwataka wachangie vizuri agenda zote zilizowasilishwa. Baada ya hayo alifungua kikao saa 3:37 asubuhi.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOL II/NA.116/2021/2022: KURIDHIA AGENDA**

Agenda ziliwasilishwa wajumbe waliridhia.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOL.II/NA.117/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAM (CMT) CHA TAREHE 09.03.2022.**

Katibu wa Kikao aliwasilisha muhtasari wa kikao cha Timu ya Wataalam cha tarehe 09.03.2022, kisha Mwenyekiti akawapatia wajumbe nafasi ya kupitia ukurasa kwa ukurasa ambapo wajumbe waliridhia muhtasari usainiwe kwa ajili ya kumbukumbu za kiofisi.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOL.II/NA.118/2021/2022: YATOKANAYO NA KIKAO CHA TIMU YA WATAALAM (CMT) CHA TAREHE 09.03.2022.**

Taarifa iliwasilishwa wajumbe wakaipokea na kujadili waliagiza yafuatayo yatekelezwe;

a) POs zipelekwe Kata ya Ipande (Damwelu), Chabutwa, Muhanga, Kalangali ili makusanyo ya mapato.
b) Yawasilishwe mapendekezo ya vyanzo vipya vya mapato na maeneo ambayo hayakusanyi.
c) Mgambo aliyepo mmoja apangiwe majukumu ya kazi kwa kipindi cha Mwezi mmoja na makubaliano ya malipo yafanyike hadi kufikia tarehe 17.04.2022 mgambo aanze kazi.
d) Iwasilishwe taarifa ya mchanganuo wa matumizi ya fedha na kiasi kilichozidi kwenye ujenzi wa Zahanati ya Mbugani, Kazikazi na Kamenyanga na ikiwa fedha zilizidi zilitoka wapi.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOL II/NA.119/2021/2022: KUSOMA NA KUREKEBISHA MIHTASARI YA VIKAO VYA KAMATI MBALIMBALI.**

Katibu aliwasilisha mihtasari ya kamati mbaimbali baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa wajumbe walishauri marekebisho yafanyike na mihtasari iwasilishwe kwenye kamati husika. Idha Katibu wa Mbunge asihudhurie vikao kwa kuwa yeye si mjumbe na hajapishwa. Kuhusu hoja za ukaguzi kifanyike kikao kati ya Mkurugenzi Mtendaji, Afisa Utumishi, Afisa Elimu Msingi na Sekondari, Afisa Sheria na Mkaguzi wa Ndani ili kufuta hoja ya mikataba ambayo haikufanyiwa upekuzi.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.120/2021/2022: TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWEZI MACHI, 2021.**

Mweka Hazina aliwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya mwezi Machi, 2022 kama ifuatavyo:

**A: MAPATO**

Katika mwaka wa fedha **2021/2022** Halmashauri ya Wilaya ya Itigi imekadiria kukusanya na kutumia jumla ya Tshs 18,284,649,098.00 ikiwa ni ruzuku ya mishahara (P.E) Tshs 8,881,696,000.00, Ruzuku ya matumizi ya kawaida (O.C) Tshs 1,088,069,000.00 Ruzuku ya fedha za miradi ya maendeleo (Dev Grants) Tshs 6,410,893,265.00 na mapato ya ndani (Own Source) Tsh 1,903,990,833.00 kwa mchanganuo ufuatao;

**JEDWALI 1: MAKADIRIO YA MAPATO NA MAPATO HALISI**

| | CHANZO CHA MAPATO | MAKADIRIO 2021/2022 | MAPATO MACHI, 2022 | MAPATO JULAI-MACHI, 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| MAPATO YA NDANI | Mapato Halisi | 1,735,560,000.00 | 91,068,614.91 | 1,118,147,226.30 | 64.43 |
| | Mapato Lindwa | 168,430,833.00 | 13,163,679.70 | 77,895,102.74 | 46.25 |
| | **Jumla Ndogo** | **1,903,990,833.00** | **104,232,294.61** | **1,196,042,329.04** | **62.82** |
| RUKUZU | Mishahara-Ruzuku | 8,881,696,000.00 | 682,695,000.00 | 6,348,108,220.00 | 71.47 |
| | Matumizi ya Kawaida (OC) | 1,088,069,000.00 | 61,395,749.99 | 662,019,409.45 | 60.84 |
| | Miradi ya Maendeleo | 6,410,893,265.00 | 511,141,548.30 | 6,611,459,727.21 | 103.13 |
| | **Jumla Ndogo** | **16,380,658,265.00** | **1,255,232,298.29** | **13,621,587,356.66** | **83.16** |
| JUMLA | **Jumla Kuu** | **18,284,649,098.00** | **1,359,464,592.90** | **14,817,629,685.70** | 81.04 |

**JEDWALI 2: MAKADIRIO YA MATUMIZI NA MATUMIZI HALISI**

| | CHANZO CHA MATUMIZI | MAKADIRIO 2021/2022 | MATUMIZI MACHI, 2022 | MATUMIZI JULAI, 2021-MACHI, 2022 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| MATUMIZI YA KAWAIDA | Mapato ya Ndani | 1,147,905,970.00 | 49,782,135.79 | 856,356,972.35 | 74.60 |
| | Ruzuku-OC | 1,088,069,000.00 | 36,610,000.00 | 509,671,664.00 | 46.84 |
| | **Jumla Ndogo** | **2,253,835,833.00** | **86,392,135.79** | **1,460,026,039.56** | **64.78** |
| | Ruzuku ya Mishahara Serikali | 8,881,696,000.00 | 682,695,000.00 | 5,645,279,220.00 | 63.56 |
| | Mishahara OS | 17,860,863.00 | 971,700.00 | 12,303,328.99 | 68.88 |
| | **Jumla Ndogo** | **8,899,556,863.00** | **683,666,700.00** | **6,347,812,855.88** | **71.47** |
| MIRADI YA MAENDELEO | Mapato Ndani | 738,224,000.00 | 55,000,000.00 | 205,975,633.00 | 27.90 |
| | Ruzuku Serikali Kuu, Wahisani | 6,410,893,265.00 | 889,735,345.74 | 5,516788,496.15 | 86.05 |
| | **Jumla Ndogo** | **7,149,117,265.00** | **944,735,345.74** | **5,722,764,129.15** | **80.05** |
| | **Jumla Kuu** | **18,284,649,098.00** | **1,714,794,181.53** | **12,534,308,052.50** | **68.55** |

Baada ya kuipitia taarifa hii ukurasa kwa ukurasa mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe ili waweze kujadili wajumbe walishauri kuingiza taarifa ya mapokezi ya fedha za MSD kwenye taarifa ya mapato na matumizi pamoja na kushirikisha Idara au Kitengo husika wanapotaka kulipa kwa kutumia vifungu vya Idara au Kitengo husika.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.121/2021/2022: TAARIFA ZA IDARA NA VITENGO MBALIMBALI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI-MACHI, 2021**

- **IDARA YA FEDHA NA BIASHARA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Fedha na Biashara kwa kipindi cha Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni kuandaa taarifa za mapato na matumizi za kila mwezi, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa vyanzo vyake vya ndani ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2021-Machi, 2022 Halmashauri imekusanya Tshs 1,196,042,329.04 sawa na 62.82% ya lengo la mwaka Tshs 1,903,990,833.00, pia Halmashauri imekuwa na timu ya ufuatiliaji wa mapato ili kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa na kuzuia utoroshaji wa mapato hasa ushuru wa mazao, madini ya ujenzi, leseni za biashara, ushuru wa huduma, ushuru wa nyumba za kulala wageni, kusimamia upelekaji wa fedha katika ngazi za kutolea huduma za afya, elimu, vikundi na usimamizi wa usuluhishi wa kibenki kwa kila mwezi. Aidha, taarifa ilieleza changamoto ambazo Idara inakumbana nazo pamoja na mikakati ya utatauzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa na baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa mjumbe alishauri wanaotengeneza barabara watozwe ushuru wa madin ya ujenzi. Afisa Mazingira alieleza kuwa wanaotengeneza barabara wameingia makubaliano na mwenye eneo, na baada ya mradi kukamilika wanalipa gharama za kufukia mashimo au kuyafukia. Afisa Sheria alieleza kuwa makubaliano yalifanyika na kampuni inayotengeneza barabara waliomba kusamehewa ushuru wa madini ya ujenzi ila walikubaliana kutoa huduma ya kupeleka madini ya ujenzi katika miradi pale itakapo hitajika. Baada ya majadiliano ya kina waliazimia yafuatayo;

a) Iandikwe barua kwa Afisa Madini Mkazi kuonesha kuwa hakuna mawasiliano yaliyofanyika kuweka mgodi wa uchimbaji madini ya ujenzi kwenye eneo ambalo limepimwa ambalo lipo katikati ya mji pamoja na kutoa leseni ya uchimbaji wa madini ya ujenzi pasipo kushirikisha Halmashauri.
b) Aandikiwe barua mmiliki wa leseni ya mgodi wa madini ya ujenzi ili aitwe kutoa maelezo kuhusu eneo analotumia kutoa madini ya ujenzi.

- **IDARA YA MIPANGO, TAKWIMU NA UFUATILIAJI**

Taarifa ya Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kuandaa na kuwasilisha taarifa mbalimbali za utekelezaji, kuratibu maandalizi ya awali ya zoezi la Sensa ya watu na makazi, kuratibu uandaaji wa nyaraka za kuombea fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/22, kuhakikisha fedha zinazotolewa bila kuwa na vifungu vya matumizi zinaombewa vifungu ili ziweze kutumika, kuratibu maandalizi ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023, Aidha, taarifa ilieleza changamoto ambazo Idara inakumbana nazo mojawapo ni ushiriki mdogo wa wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo hasa katika miradi iliyopata fedha kutoka Serikali Kuu na kwa Wahisani, mabadiliko ya bei ya bidhaa za ujenzi na bei za mafuta, kutokufikika kirahisi kwa baadhi ya maeneo yenye miradi kutokana na umbali na hivyo kuathiri ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji, makusanyo ya mapato ya ndani kuwa madogo.Taarifa ilionesha mikakati ya utatauzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Utumishi na Utawala kwa kipindi cha Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na mapokezi ya mtumishi mmoja (1) ambaye ni Muuguzi Daraja II, Watumishi watatu (3) wamehamia na Watumishi nane (8) wamehama Halmashauri ya Wilaya ya Itigi, Watumishi wanne (4) wamekoma Utumishi, ambapo watumishi watatu (3) wamestaafu na Mtumishi mmoja amefukuzwa kazi kutoka Idara ya Elimu Msingi. Wajumbe walipitia taarifa ukurasa kwa ukurasa na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA –SEHEMU YA USAFIRISHAJI**

Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Idara ya Utumishi na Utawala-Sehemu ya Usafiri kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na kuratibu na kupanga safari za magari, pikipiki na mitambo, kufuatilia na kusimamia matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kusimamia uendeshaji na uegeshaji wa magari, kutoa taarifa ya hali ya vyombo vya usafiri na mitambo ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri imepokea pikipiki mbili aina ya Boxer STM 242 na STM 243 kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za mifugo zilizotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na tayari wamepewa Maafisa Ugani Kata ya Mitundu na Kitaraka. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA MAENDELEO YA JAMII**

Taarifa ya Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha robo ya tatu Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali vya wanawake na vijana ambapo jumla ya Tshs 17,778,900 zilikusanywa, usajili na utambuzi wa vikundi ishirini na nne (24) vya wanawake , vijana na watu wenye ulemavu, vikundi vilivyoomba mkopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu ambapo jumla ya vikundi 74 vimeomba mkopo wenye thamani ya Tsh 627,091,500 kati ya hivyo vikundi vya vijana ni 22 na vikundi vya

wanawake ni 49, watu wenye ulemavu vikundi 2 na wazee kikundi kimoja, Utoaji wa elimu ya mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali, mafunzo ya ufugaji wa Nyuki na kilimo cha bustani (Hotculture), Mafunzo kwa wahamasishaji jamii kuhusu huduma ya tohara na maadhinisho ya siku ya wanawake Duniani iliyofanyika tarehe 8.03.2022 katika Kata ya Tambukareli. Wajumbe waliipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA KUDHIBITI UKIMWI**

Taarifa ya utekelezaji ya Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo ilieleza shughuli zilizofanyika ni pamoja na;

i. Jumla ya mipira (Kondom) 3500 ya kiume imesambazwa katika nyumba 15 za kulala wageni, sehemu 11 za starehe (bar) na katika stendi ya mabasi Itigi na Mitundu. Aidha, usambazaji unaedelea.
ii. Elimu imetolewa juu ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kupitia vikundi vya wajasiriamali na kwa walengwa wa TASAF.
iii. Idara kwa kushirikiana na shirika la APHTA limeendelea kufanya uhamasishaji kwa jamii juu ya utoaji huduma ya Tohara salama bure kwa vijana wa kiume wenye umri kuanzia miaka 15 na kuendelea.
iv. Usimamizi shirikishi juu ya huduma za UKIMWI zimefanyika katika vituo 10 vya tiba na matunzo

Wajumbe walipokea taarifa hii baada kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA TASAF**

Taarifa ya utekelezaji kazi za Kitengo cha TASAF kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na uhawilishaji wa malipo ya fedha za walengwa wa TASAF III kwa kipindi cha Mwezi Julai-Agosti na Septemba –Oktoba, 2021. Jumla ya fedha zilizoolewa kwa ajili ya malipo ni Tshs 231,609,044 sawa na kaya 3,363. Kaya 3305 zililipwa sawa na Tshs 227,711,044/= na kaya 58 hazikulipwa sawa na Tshs 3,898,000/=. Jumla ya walengwa 214 walilipwa kwa njia ya elekroniki yaani kupitia huduma za kibenki na mitandao ya simu kwenye vijiji vya Itigi Mjini, Mlowa, Tambukareli, Songambele na Majengo. Walengwa wanaolipwa kwa njia ya taslimu, benki na mitandao ya simu watalazimika kufika Ofisi za Vijiji husika wanapoishi ili waweze kuchukua risiti za malipo na kusaini kwenye orodha ya walengwa wanaolipwa ili kuthibitisha uwepo wao na kukiri kupokea fedha. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA ELIMU MSINGI**

Taarifa ya utekelezaji kazi za Idara ya Elimu msingi kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja ufuatiliaji wa maendeleo ya taaluma shuleni, ufuatiliaji na uhakiki wa miradi ya UVIKO-19, kuombea usajili Vituo Shikizi 12 kati ya 25 vilivyokidhi vigezo ili viweze kupata usajili, uendeshaji wa mtihani wa utamilifu Mkoa kwa darasa VII 2022 na darasa la IV 2022, kufanya ubainishaji wa watoto wenye ulemavu kwa Kata zote na kubaini jumla ya watoto 34 wenye ulemavu na wengine wamepatiwa ushauri wa kupata matibabu. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA ELIMU SEKONDARI**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Idara ya Elimu Sekondari kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo Idara imefanya shughuli mbalimbali ambazo ni mapokezi ya wanafunzi 1562 kati ya 2205 waliopangiwa wa kidato cha kwanza ikiwa ni sawa na 71% ya wanafunzi wote walioripoti, ufuatiliaji wa ujenzi wa miradi, ujenzi umekamilika kwenye shule 10 ambapo zoezi la utengenezaji wa viti na meza unaendelea kwenye shule hizo, maandalizi ya ukusanyaji na ujazaji wa takwimu za shule za Sekondari (TSS), kufanya maandalizi ya mtihani wa utamilifu kidato cha nne, kupokea matokeo ya kidato cha pili na cha nne, 2021.Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA USAFI NA MAZINGIRA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara kwa kipindi cha robo ya tatu Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo ilijumuisha usimamizi na ukaguzi wa usafi wa mazingira kwa kila wiki siku ya Jumatano na kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi, ukaguzi wa hali ya miundombinu ya usafi hususani maeneo ya kukusanyia taka ngumu, zoezi la upandaji miti na ugawaji miti kwa taasisi za Serikali na za dini, ukaguzi kwenye maeneo ya uchakataji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali, ukaguzi wa mazingira kwenye maeneo ya shule za msingi hususani vituo shikizi 18 na shule za sekondari 5 lengo nikuanza kutoa huduma ambazo zitazingatia utunzaji wa Mazingira, kuratibu na kusimamia ujenzi wa mradi wa shule ya sekondari Kitaraka, kusimamia na kufanya ukaguzi wa kitalu cha miche Shule ya Sekondari Kimadoi kwa awamu ya pili baada ya kuzalisha miche zaidi ya 10,000 kwa awamu ya kwanza. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA MIFUGO NA UVUVI**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na tiba kwa mifugo, kinga za magonjwa ya mifugo, ukaguzi wa nyama, kutoa elimu na ushauri juu ya uboreshaji wa mifugo na mazao yatokanayo na mifugo, usimamizi wa shughuli za minada, usafirishaji wa mifugo hai, uogeshaji wa mifugo kwenye majosho, ukaguzi wa mabwawa ya samaki. Wajumbe walipitia taarifa ukurasa kwa ukurasa na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA**

Taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika kwa kipindi cha Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni usimamizi wa kilimo cha pamba kwa msimu wa mwaka 2021/2022, usambazaji wa mbegu za alizeti za ruzuku ya Serikali kwa kuuza, kukopesha kwa wakulima katika Kata na Vijiji, Usimamizi wa mafunzo ya kilimo kwa ujumla kwa vijana kwa kutumia teknolojia ya kitalu nyumba(Green House), usimamizi wa kilimo cha korosho katika Halmashauri na kilimo cha tumbaku katika Kata ya Mitundu na Mgandu. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA UJENZI**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara ya Ujenzi katika kipindi cha robo ya tatu kuanzia mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizofanyika ni pamoja na usimamizi wa nyumba sita (6) za Watumishi na nyumba ya Mkurugenzi Mtendaji ambapo utekelezaji unafanyika kwa njia ya "Force Account" kwa gharama ya Tshs 470,000,000.00, usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo ni ujenzi wa madarasa 147 katika vituo shikizi utekelezaji umefikia 85%, ujenzi wa vyumba 29 vya madarasa katika Shule za Sekondari ambapo ujenzi umekamilika. Aidha, ujenzi wa shule ya Sekondari Kitaraka unaendelea, kusimamia ukarabati wa Kituo cha Afya Mitundu ambapo kiasi cha Tshs 250,000,000/= kilipokelewa na ujenzi upo 85%. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA AFYA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Idara ya Afya kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo Halmashauri imepokea dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Tshs 928,639.03 kwa vituo viwili tu Zahanati ya Muhanga na Kituo cha Afya Itigi. Taarifa ilieleza magonjwa 10 ambayo yanaongoza kwa wagonjwa wa nje ni pamoja na magonjwa ya mfumo wa hewa, magonjwa ya kuhara, magonjwa ya mfumo wa mkojo, magonjwa mengine ya mfumo wa chakula, malaria, magonjwa mengineyo, homa ya vichomi, magonjwa mengineyo ya upasuaji, magonjwa ya ngozi ambayo sio fangasi na minyoo. Wajumbe walipokea taarifa na baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **IDARA YA ARDHI NA MALIASILI**

Taarifa ya Utekelezaji wa kazi za Idara kwa kipindi cha robo ya tatu kuanzia mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa shughuli zilizofanyika ni pamoja na kushughulikia taarifa za wanyamapori waharibifu wa mal na tishio kwa maisha ya wananchi, Elimu ya uhifadhi, usimamizi wa matumizi endelevu ya wanyamapori. Jumla ya Tshs 950,000.00 zimekusanywa kutokana na mauzo ya wanyamapori waharibifu wa mazao ya wananchi. Halmashauri imepokea Tshs 24,913,600.00 za mgawo wa mapato ya uwindaji wa kitalii (25%) kwa msimu wa uwindaji wa mwaka 2021/2022. TAWA pori la Akiba la Rungwa Kizigo na Muhesi. Vijiji 14 vinavyopakana na Vitalu vya uwindaji vimepata mgawo wa dola 30,000 sawa na Tshs 54,007,000.00, kila kijiji kimepata wastani Tshs 3,850,000.00 na fedha hizi zimependekezwa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika vituo Shikizi. Halmashauri imepokea na kuanza utekelezaji wa mradi wa kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wakati walio kwenye mnyororo wa thamani wa zao la asali ili waweze kuyafikia masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kupitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA MANUNUZI NA UGAVI**

Taarifa ya kitengo cha Manunuzi na Ugavi kwa kipindi cha robo ya tatu kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 ambapo Halmashauri imekisia kutumia Tshs 8,379,534,617.43 kati ya hizo Tshs 4,513,151,562.12 ni bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na Tshs 3,912,500,000.00 ikiwa ni feha za nyongeza ya bajeti ya fedha za UVIKO-19, TEA na Tozo katika manunuzi ya bidhaa, huduma na kazi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwenye Idara na Vitengo mbalimbali kwa gharama ya Tshs 162,463,223.67. Aidha, kwa kipindi cha Julai 2021 hadi Machi, 2021 Halmashauri imetumia jumla ya Tsh 758,000,703.93 sawa na 9% ya mpango wa manunuzi.

Ufuatao ni mchanganuo wa taarifa ya manunuzi;

| NA. | AINA YA UNUNUZI | MAKISIO | UTEKELEZAJI | | JUMLA | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | JULAI 2021-DISEMBA 2021 | JANUARI 2022-MACHI, 2022 | | |
| 1. | Ununuzi wa Vifaa | 7,435,226,593.43 | 483,636,346.12 | 125,190,936.77 | 608,827,282.89 | 8 |
| 2. | Huduma zisizo za kitaalam | 221,750,000.0 | 60,565,571.38 | 36,322,286.90 | 96,887,858.28 | 44 |
| 3. | Huduma za Kitaalam | 35,683,024.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 4. | Kazi | 686,875,000.00 | 51,335,562.76 | 950,000.00 | 52,285,562.76 | 8 |
| | **Jumla Kuu** | **4,513,151,562.12** | **595,537,480.26** | **162,463,223.67** | **758,000,703.93** | 9 |

Taarifa ilieleza changamoto pamoja na ufumbuzi wa changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA UCHAGUZI**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha Uchaguzi katika kipindi cha robo ya tatu Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo shughuli zilizofanyika ni kuandaa taarifa ya vituo vitakavyotumika katika uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura litakalofanyika baada ya kukamilika kwa zoezi la sense ya watu na makazi na kuwasilisha Mkoani. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA TEHAMA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha TEHAMA kwa kipindi cha Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo kitengo kimeendelea kusimamia mifumo mbalimbali inayopatikana kwenye miundombinu ya Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na kutoa mafunzo ya mfumo mpya wa malipo kwa kutumia kumbukumbu namba ya malipo (Control No.) kwenye malipo ya ICHF ambapo mafunzo yalitolewa kwa waandikishaji, wasimamizi wa vituo pamoja na wasimamizi wa Kata. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

- **KITENGO CHA SHERIA**

Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kitengo cha Sheria kwa kipindi cha Mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa ambapo ilijumuisha shughuli mbalimbali zilitekelezwa ambazo ni kuishauri Halmashauri na wananchi masuala mbalimbali ya kisheria ikiwa ni pamoja na kutatua mgogoro wa muda mrefu kati ya Halmashauri na wahanga 11 wa viwanja vilivyotwaliwa na kuanzisha stendi ya mabasi kwa kuandaa mchakato, kusaini mikataba ya fidia ya viwanja na kukabidhi viwanja hivyo. Kufanyia upekuzi mikataba mbalimbali, kufuatilia sheria ndogo na kanuni za kudumu ambapo tayari zimetangazwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 04.03.2022 hivyo Halmashauri inapaswa kulipia nakala kwa mahitaji husika kwa matumizi ya Ofisi, kutoa mafunzo ya uapishaji wa mabaraza ya Kata na ardhi ya Vijiji. Aidha, Afisa Sheria aliwaeleza wajumbe kuhusu kesi Na. 01 ya mwaka 2022 dhidi ya Halmashauri kuhusu ununuzi wa kadi za CHF kutoka kwa mzabuni Lot General Suppliers. Afisa Ugavi aliwaeleza wajumbe kuwa mzabuni alileta vifaa ambavyo vilipokelewa pasipo kufuata utaratibu. Afisa Sheria aliwashauri kumlipa mzabuni madai yake ili afute kesi mahakamani. Wajumbe waliazimia kuwa Mkurugenzi akae kikao na Afisa Sheria, Mweka Hazina, Mganga Mkuu na Afisa Manunuzi na Ugavi ili kuona namna ya kujibu kesi ya mzabuni huyo.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.122/2021/2022: OMBI LA KIBALI CHA AJIRA YA KUJITOLEA.**

Afisa Utumishi aliwasilisha ombi la kibali cha ajira ya kujitolea ambapo aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi inaupungufu wa Watumishi katika Sekta mbalimbali kupitia Idara zote. Halmashauri inahitaji kuwa na Watumishi 1906 lakini ina watumishi 886 hivyo ina upungufu wa Watumishi 1020. Aliomba kuruhusu Watumishi ambao wataomba kujitolea katika sekta zifuatazo bila malipo kwa kuwa hakuna fungu la mishahara ya kuwalipa ili waweze kusaidia utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Halmashauri. Sekta hizo ni;

i. Utawala- Madereva, Masijala ya wazi, Watendaji wa Vijiji.
ii. Maliasili- Nyuki, afisa Wanyama pori, Mhifadhi wanyama pori
iii. Ujenzi- Wahandisi, Fundi Sanifu
iv. Kilimo- Afisa Kilimo, Afisa Kilimo Msaidizi na wataalam wa Umwagiliaji
v. Mifugo- Afisa MIfugo, Afisa Mifugo Msaidizi
vi. Kitengo cha habari- Mwandishi wa Habari

Aidha, kwa sekta zingine wapewe kibali cha miezi mitatu mitatu kwa ajili ya kupata ujuzi. Wajumbe walipokea na waliridhia ombi hili na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.123/2021/2022: MAPENDEKEZO YA UTEUZI WA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.**

Afisa Utumishi aliwasilisha mapendekezo ya uteuzi wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira kwa kuwa Mwenyekiti aliyekuwepo kamaliza muda wake wa miaka mitano muda mrefu na Halmashauri ilikuwa ikitangaza bila kupata waombaji mpaka iliporudia kutoa Tangazo lenye Kumb. Na HW/ITG/S.1/5/VOL.ii la tarehe 16 Februari, 2022 na kupokea maombi ya watu wawili ambao ni Reuben John Nambasita (umri 72) Mkazi wa Sanjaranda Elimu yake ni darasa la nane na anacheti cha mafunzo ya Ualimu Kazini (MUKA) pia ni Mwalimu Mstaafu na Donald M. Lupaa (umri 62) Mkazi wa Itigi Majengo, Elimu yake ni kidato cha sita na ujuzi wa shahada ya Uamili ya Utawala na Stashahada ya juu ya usimamizi Rasilimali watu. Wajumbe baada ya kupitia mapendekezo haya walimpendekeza ndugu Donald m. Lupaa kua Mwenyekiti wa Bodi ya Ajira.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.124/2021/2022: MAPENDEKEZO YA KUBADILISHA JINA LA JIMBO LA UCHAGUZI.**

Afisa Uchaguzi aliwasilisha mapendekezo ya kubadilisha jina la Jimbo la Uchaguzi kutoka jina la awali Jimbo la Manyoni Magharibi na jina jipya ni Jimbo la Itigi. Mabadiliko ya jina la jimbo yataondoa Mkanganyiko uliokuwa ukijitokeza wakati wa upokeaji wa nyaraka na vifaa mbalimbali vya uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 kutokana na kufanana majina ya jimbo la Manyoni Mashariki na Manyoni Magharibi. Wajumbe walipokea mapendekezo haya na waliridhia jina jipya la Jimbo la Itigi.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.125/2021/2022: TAARIFA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MFUKO WA AFYA WA PAMOJA (HSBF) NA UNICEF KWA AJILI YA VYETI VYA WATOTO.**

Mganga Mkuu aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za Mfuko wa Afya wa pamoja (HSBF) Tshs 70,134,992.94, Fedha za UNICEF kwa ajili ya vyeti vya watoto kipindi cha Januari-Juni kiasi cha Tshs 5,000,000.00, Fedha za Mfuko wa Afya wa Dunia (Global Fund) Tshs 1,413,658.05 na malipo ya kugharamia ajira ya mkataba wa miezi 6 kuchochea mapambano dhidi ya UVIKO-19 Tshs 3,458,560.00, Jumla ya mapokezi ya fedha zote ni Tshs 80,007,560.44. Wajumbe walipokea taarifa hii na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.126/2021/2022: KUFANYA MABADILIKO YA UJENZI WA NYUMBA ZA WATUMISHI ILI KUJENGA NYUMBA YA MKURUGENZI YENYE GOROFA MOJA.**

Afisa Mipango alieleza kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri imetengewa fedha Tshs 150,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba (3) za Watumishi. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilipokea fedha na kufanya ujenzi wa nyumba 7 za Watumishi ambapo nyumba moja ilipendekezwa itumiwe na Mkurugenzi Mtendaji. Halmashauri inaomba idhini ya kutumia Tshs 150,000,000.00 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine za Watumishi zitumike kujenga nyumba ya ghorofa 1 ya Mkurugenzi Mtendaji katika eneo la maegesho ya malori lililopo Kata ya Itigi Majengo. Sababu ya kujenga katika eneo la maegesho ya malori ni kuongeza ulinzi wa maeneo ya Serikali ili kuepusha uvamizi wa wananchi na pia kuendelea kupanua maendeleo ya mji wa Itigi. Wajumbe walipokea taarifa hii, waliridhia na hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.127/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI NYUMBA ZA WATUMISHI.**

Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi nyumba za Watumishi ambapo Halmashauri ilitengewa fedha kiasi cha Tshs 558,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nane za Watumishi sawa na wastani wa Tshs 69,750,000.00 kwa nyumba moja. Kiasi cha Tshs 470, 287,425.83 kilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Watumishi na hivyo kupelekea idadi ya nyumba kupungua kutoka nane hadi saba. Kiasi hiki kilikuwa pungufu kwa Tshs 17,962,574.17 ukilinganisha na makadiio ya bajeti ya ujenzi wa nyumba saba ambapo ilipaswa kufikia kiasi cha Tshs 488,250,000.00. Mradi kwa sasa upo hatua ya ukamilishaji sawa na 98% ya utekelezaji ambapo kiasi cha Tshs 470,287,425.83 sawa na 100% ya fedha iliyoyolewa imetumika. Fedha iliyotumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa ni Tshs 404,710,072.73 na malipo ya mafundi Tshs 65,577,353.10, pamoja na matumizi hayo zipo shughuli ambazo utekelezaji wake bado kukamilika ambazo ni;

| | | |
|---|---|---|
| i. Uwekaji wa vigae maeneo ambayo bado | Tshs | 1,200,000.00 |
| ii. Ukamilishaji wa mashimo ya maji taka | Tshs | 2,500,000.00 |
| iii. Malipo ya gharama za uingizaji umeme na vifaa | Tshs | 4,539,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| iv. | Ununuzi wa vifaa vya mfumo wa maji | Tshs 1,757,500.00 |
| v. | Mfumo wa upoozaji wa hewa (Air Conditioner) | Tshs 1,900,000.00 |
| vi. | Ukamilishaji wa dali | Tshs 670,000.00 |
| vii. | Ufundi | Tshs 16,956,969.10 |
| | **Jumla Kuu** | **Tshs 29,523,469.10** |

Wajumbe walipokea taarifa na walishauri kifungu cha malipo kitoke kwenye kifungu cha ujenzi wa vizimba.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.128/2021/2022: OMBI LA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA TSHS 13,661,988.00.**
Mweka Hazina aliwasilisha ombi la kubadili matumizi ya fedha Tshs 13,661,988.00, wajumbe walipokea na waliridhia kubadili matumizi hayo kama yalivyoombwa.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.129/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU 2021/2022.**
Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya tatu kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 ambapo Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tshs 7,149,117,265.00 katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo fedha toka Serikali kuu 2, 583,057,000.00, Mapato ya Ndani Tshs 738,224,000.00 na Wadau Mbalimbali wa Maendeleo Tshs 3,827,836,265.00. Hadi kufikia tarehe 15, Machi, 2022 fedha za miradi zilizopokelewa toka Serikali Kuu, Wadau wa Maendeleo na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni Tshs 6,821,262,212.23 sawa na 95% ya makisio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ni pamoja na kuchelewa kwa upatikanaji wa vifungu kwa fedha zinazokuja nje ya bajeti na fedha zinazohitaji uhamisho wa vifungu, makusanyo ya mapato ya ndani kuwa madogo kutokana na kuwepo vyanzo vichache vya mapato, ushiriki mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa miradi inayopata fedha za ruzuku, mabadiliko ya bei ya bidhaa za ujenzi na bei za mafuta ambapo zinapelekea kuongeza gharama za uendeshaji wa miradi. Aidha, taarifa ilionesha mikakati mbalimbali ili kuweza kutatua changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.130/2021/2022: TAARIFA YA HALI YA USALAMA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI-MACHI, 2022.**
Taarifa ya hali ya usalama kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa, wajumbe walipokea taarifa na baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.131/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**
Hakuna Mengineyo.

**MUHT/HW/ITG/VOLII/NA.132/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuchangia agenda zote kwa umakini. Alifunga kikao saa 10:35 jioni.

**UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA,**

............................
Joyce J. Masoga
**Katibu**
Tarehe **09.05.2022**

............................
John K. Mgalula
**Mwenyekiti**
Tarehe **09.05.2022**

| | | |
|---|---|---|
| iv. | Ununuzi wa vifaa vya mfumo wa maji | Tshs 1,757,500.00 |
| v. | Mfumo wa upoozaji wa hewa (Air Conditioner) | Tshs 1,900,000.00 |
| vi. | Ukamilishaji wa dali | Tshs 670,000.00 |
| vii. | Ufundi | Tshs 16,956,969.10 |
| | **Jumla Kuu** | **Tshs 29,523,469.10** |

Wajumbe walipokea taarifa na walishauri kifungu cha malipo kitoke kwenye kifungu cha ujenzi wa vizimba.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.128/2021/2022: OMBI LA KUBADILI MATUMIZI YA FEDHA TSHS 13,661,988.00.**
Mweka Hazina aliwasilisha ombi la kubadili matumizi ya fedha Tshs 13,661,988.00, wajumbe walipokea na waliridhia kubadili matumizi hayo kama yalivyoombwa.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.129/2021/2022: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ROBO YA TATU 2021/2022.**
Afisa Mipango aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo robo ya tatu kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 ambapo Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tshs 7,149,117,265.00 katika kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo fedha toka Serikali kuu 2, 583,057,000.00, Mapato ya Ndani Tshs 738,224,000.00 na Wadau Mbalimbali wa Maendeleo Tshs 3,827,836,265.00. Hadi kufikia tarehe 15, Machi, 2022 fedha za miradi zilizopokelewa toka Serikali Kuu, Wadau wa Maendeleo na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni Tshs 6,821,262,212.23 sawa na 95% ya makisio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa miradi ni pamoja na kuchelewa kwa upatikanaji wa vifungu kwa fedha zinazokuja nje ya bajeti na fedha zinazohitaji uhamisho wa vifungu, makusanyo ya mapato ya ndani kuwa madogo kutokana na kuwepo vyanzo vichache vya mapato, ushiriki mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa miradi inayopata fedha za ruzuku, mabadiliko ya bei ya bidhaa za ujenzi na bei za mafuta ambapo zinapelekea kuongeza gharama za uendeshaji wa miradi. Aidha, taarifa ilionesha mikakati mbalimbali ili kuwe a kutatua changamoto hizo. Wajumbe walipokea taarifa baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.130/2021/2022: TAARIFA YA HALI YA USALAMA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI-MACHI, 2022.**
Taarifa ya hali ya usalama kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2021 iliwasilishwa, wajumbe walipokea taarifa na baada ya kuipitia ukurasa kwa ukurasa hapakuwa na hoja iliyojitokeza.

**MUHT/HW/ITG/KTW/VOLII/NA.131/2021/2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI.**
Hakuna Mengineyo.

**MUHT/HW/ITG/VOLII/NA.132/2021/2022: KUFUNGA KIKAO.**
Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga kikao, Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kuchangia agenda zote kwa umakini. Alifunga kikao saa 10:35 jioni.

**UMETHIBITISHWA NA KUSAINIWA NA,**

......................
Joyce J. Masoga
**Katibu**
Tarehe **09.05.2022**

......................
John K. Mgalula
**Mwenyekiti**
Tarehe **09.05.2022**

**KWENDA KWA: MHE. MWENYEKITI,**

**KUH: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO HADI KUFIKIA ROBO YA TATU (JULAI 2021/MACHI 2022) YA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika Bajeti ya Mwaka wa fedha 2021/2022, Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha **TZS. 7,149,117,265.00** katika kutekeleza Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Kiasi hiki cha fedha kinatokana na: -

| ***CHANZO*** | ***TSHS*** |
|---|---|
| • Serikali kuu........................................................ | **2,583,057,000.00** |
| • Mapato ya ndani.................................................. | **738,224,000.00** |
| • Wadau mbalimbali wa Maendeleo.............................. | **3,827,836,265.00** |

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

Hadi kufikia tarehe 15 Machi, 2022, fedha za miradi zilizopokelewa toka Serikali Kuu, Wadau wa maendeleo na mapato ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya Maendeleo ni **TZS. 6,821,262,212.23** sawa na **asilimia 95** ya makisio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 kama inavyoonekana katika **jedwali Na.1**.

**Jedwali 01: Muhtasari wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kuanzia Julai hadi tarehe 15 Machi 2022**

| NA. | CHANZO CHA FEDHA | MAKISIO KWA MWAKA 2021/2022 | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | SALIO | % TUMIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Halmashauri katika Miradi- (Own source) | 738,224,000.00 | 240,263,132.60 | 195,284,132.60 | 44,979,000.00 | 81 |
| 2 | Mfuko wa Jimbo | 54,324,000.00 | 54,324,000.00 | 21,500,000.00 | 32,824,000.00 | 40 |
| 3 | Ujenzi wa Nyumba za Watumishi | 150,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 4 | Ujenzi wa maboma – Elimu Msingi | 112,500,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 5 | Ujenzi wa maboma – Elimu Sekondari | 262,500,000.00 | 275,000,000.00 | 130,416,029.00 | 144,583,971.00 | 47 |
| 7 | Ujenzi wa Zahanati | 150,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 8 | Ujenzi wa Vituo vya Afya | 300,000,000.00 | 250,000,000.00 | 138,767,489.44 | 111,232,510.56 | 56 |
| 9 | Ujenzi wa Hospitali | 500,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 10 | SEQUIP T | 985,200,000.00 | 470,000,000.00 | 90,985,980.69 | 379,014,019.31 | 19 |
| 11 | SRWS - Msingi | 300,000,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |

| NA. | CHANZO CHA FEDHA | MAKISIO KWA MWAKA 2021/2022 | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | SALIO | % TUMIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12 | EP4R – Elimu Msingi | 346,581,500.00 | 155,417,139.55 | 127,969,556.96 | 27,447,582.59 | 82 |
| 13 | EP4R – Elimu Sekondari | 346,581,500.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 14 | Mfuko wa Pamoja wa Afya (HBF) | 357,662,140.00 | 140,269,986.00 | 43,087,847.96 | 97,182,138.04 | 31 |
| 15 | UNICEF | 10,000,000.00 | 5,000,000.00 | 0.00 | 5,000,000.00 | 0 |
| 16 | GLOBAL FUND | 16,061,000.00 | 1,413,658.54 | 1,413,658.54 | 0.00 | 100 |
| 17 | NTD | 15,549,000.00 | 1,870,750.08 | 1,870,750.08 | 0.00 | 100 |
| 18 | NUTRITION | 3,536,125.00 | 1,000,000.00 | 1,000,000.00 | 0.00 | 100 |
| 19 | RBF | 323,798,000.00 | 0.00 | 0.00 | 0.00 | 0 |
| 20 | TASAF | 1,122,867,000.00 | 628,620,154.00 | 627,087,758.00 | 1,532,396.00 | 100 |
| 21 | Mitihani - Msingi | 230,611,000.00 | 230,609,180.00 | 230,609,180.00 | 0.00 | 100 |
| 22 | Mitihani - Sekondari | 175,815,000.00 | 163,010,000.00 | 163,010,000.00 | 0.00 | 100 |
| 23 | Elimu Bila Malipo - Msingi | 397,077,000.00 | 240,956,685.67 | 215,029,095.67 | 25,927,590.00 | 89 |
| 24 | Elimu Bila Malipo - Sekondari | 250,230,000.00 | 144,010,362.71 | 131,696,890.81 | 12,313,471.90 | 91 |
| 27 | IMF-UVIKO-19 | 0.00 | 3,679,565,413.00 | 3,126,305,913.39 | 553,259,499.61 | 85 |
| 29 | TEA | 0.00 | 100,000,000.00 | 0.00 | 100,000,000.00 | 0 |
| 31 | EGPAF | 0.00 | 16,931,750.08 | 16,931,750.08 | 0.00 | 100 |
| 33 | SRWSS - Afya | 0.00 | 23,000,000.00 | 23,000,000.00 | 0.00 | 100 |
| 34 | ANUANI ZA MAKAZI | 0.00 | 116,600,000.00 | 0.00 | 116,600,000.00 | 0 |
| ***JUMLA KUU*** | | ***7,149,117,265.00*** | ***6,821,262,212.23*** | ***5,285,966,033.22*** | ***1,535,296,179.01*** | **77** |

## 3.0 Changamoto na Mikakati

Utekelezaji wa Miradi hii inakadiriwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo: -

### a) Changamoto

i) Kuchelewa kwa upatikanaji wa vifungu kwa fedha zinazokuja nje ya bajeti na fedha zinazohitaji uhamisho wa vifungu.

ii) Makusanyo ya mapato ya ndani kuwa madogo kutokana na uwepo wa vyanzo vichache vya uhakika vya mapato unasababisha Miradi kushindwa kutekelezeka.

iii) Ushiriki mdogo wa jamii katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa miradi inayopata fedha za ruzuku.

iv) Mabadiliko ya bei ya bidhaa za ujenzi na bei za mafuta zinaongeza gharama za uendeshaji na utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

**b) Mikakati iliyopo**

i) Kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa fedha za miradi ili iweze kutolewa kwa wakati.

ii) Kufuatilia vyanzo vya mapato ya ndani ili shughuli zilizopangwa zitekelezwe kwa wakati.

iii) Kuendelea kuhamasissha jamii kushiriki shughuli za maendeleo.

iv) Kusimamia na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kazi zinazofanyika ziwe na tija kubwa na thamani ya fedha iwepo.

Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeambatishwa.

Naomba kuwasilisha.

R. D. Mpumba
<u>KAIMU AFISA MIPANGO (W)</u>

MKUU WA IDARA (W)
IDARA YA MIPANGO NA TAKWIMU
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI